



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA WILAYA YA BIHARAMULO

Unapojibu Tafadhali Taja:

Kumb Na./BDC/4/32/VOL.II/85

21/06/2022

**MABADILIKO YA TAREHE YA TANGAZO LA KUITWA KWENYE USAILI**

Somo hapo juu lahusika.

2. Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo anapenda kuwataarifua waombaji kazi waliotuma maombi ya kujaza nafasi wazi za Mtendaji wa Kijiji Daraja la III kuwa, kuna mabadiliko ya tarehe za usaili, badala ya tarehe **24 – 25 June, 2022** iliyotangazwa hapo awali, kwa sasa anawatangazia waombaji wote walioona majina yao kuwa, usaili utafanyika tarehe **27-28 Juni, 2022** na hatimaye kuwaajiri katika Utumishi wa Umma waombaji kazi watakaofauli usaili huo.

3. Aidha, Wasailiwa walioitwa katika usaili wanapaswa kuzingatia **mambo muhimu yafuatayo:-**

- Usaili utafanyika tarehe **27/06/2022** kuanzia saa 1:30 kwa usaili wa mchujo na usaili wa mahojiano utafanyika tarehe **28/06/2022** saa 1:30 asubuhi. (kwa **watakaofanikiwa**) katika ukumbi wa shule ya Sekondari Kagango.
- Ukaguzi wa vyeti utanza saa 1.30 asubuhi kabla ya muda wa Mtihani wa mchujo/usaili wa mahojiano kuanza.
- Kuja na kitambulisho kwa ajili ya utambuzi mfano, kitambulisho cha makazi, kupiga kura, NIDA, hati ya kusafiria n.k.
- Kuja na vyeti halisi (Original Certificate) na **HALALI** vya kuanzia kidato cha Nne, Sita na Astashahada kutegemea na sifa za Mwombaji.
- Kuja na cheti halisi cha kuzaliwa. (Original Birth Certificate).

